**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI, MITANDAO YA KIJAMII NA WADAU KUHUSU UCHAPISHAJI NA USAMBAZAJI WA MATOKEO NA TAARIFA BINAFSI ZA WATAHINIWA

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwataarifu wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari, blogu, majukwaa ya habari, mitandao ya kijamii na wadau wote, kwamba, Baraza la Mitihani linalinda faragha na taarifa binafsi za kielimu za wahitimu/wanafunzi wote waliofanya mitihani inayoendeshwa na Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 Toleo la Mwaka 2023.

Aidha, Baraza la Mitihani linatambua umuhimu wa kuwapa wananchi taarifa sahihi kuhusu maendeleo ya kielimu ya wanafunzi na watahiniwa kwa kuzingatia misingi ya Sheria, maadili na heshima kwa kulinda faragha za wanafunzi na watahiniwa husika.

Kwa kuzingatia hilo, Baraza linaendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuboresha mifumo ya TEHAMA na kuondoa matokeo ya mitihani yanayoonesha jina la mwanafunzi au mtahiniwa kutoka kwenye tovuti yake www.necta.go.tz.

Kwa muktadha huo, Baraza linawajulisha kuwa ni Kosa la jinai kwa mtu yeyote, chombo cha habari, au jukwaa lolote kuhifadhi, kuchapisha, kusambaza au kuonesha hadharani matokeo ya mtihani ya mtahiniwa/mwanafunzi kwa kutumia jina lake au taarifa nyingine zozote zinazoweza kusababisha kumtambua mwanafunzi au mtahiniwa bila idhini yake. Aidha, Baraza katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa taarifa binafsi za wanafunzi au watahiniwa halitasita kuchukua hatua za Kisheria kwa yeyote atakayekwenda kinyume na matakwa haya.

**John J. Nchimbi**
**AFISA HABARI NA UHUSIANO**

**03 Septemba, 2025**